# KISWAHILI KARATASI YA TATU

# ANSWERS

# KCSE 2010

Coordinated by KENPRO, Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E, Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com/

**30.2.3 Kiswahili Karatasi ya 3 (102/3) Mwongozo wa Kusahihishia**

1. (a) -Kufungwa
-Kunyimwa uhuru
-Alipofungwa pameharibika
-Angependa kuhama lakini hawezi
-Kuna majani mengi mbele yake lakini hawezi kuyafikia zozote 4 x 1 =4

(b) amekwisha zoea hali yaki
-Hapendi kuonekana tofauti. Hataki kuukosa utu kwa sababu amefungwa katika kamba ya utu.
2 x 1=2

(c) Ni dhamiri katika nafsi yake ambayo ameshikilia ambayo haionekani kwa macho ndiyo iliyomfunga (alama 2)

(d) (i) Tashbihi -kama mbuzi
-Kama mbwa
(ii) Istiari/sitiari -Sahani ya mbingu, kamba isiyoonekana
Kutaja- 1
Kutoa mfano- 1
(iii) Tasfida - Nimekwishapachafua Zozote 2 x 2=4

(e) Mishata: Mishororo ambayo maana yake inakamilika katika mshororo unaofuata
Mf: Nami kwa mbaya bahati, katika uhuru kupigania kamba ni fupi na nimekwishachora duara.
Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, Sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena
Nami sasa sitaki ikatike maana
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba

4

(f) Nimefungwa kama mbwa na kwa bahati mbaya katika kutaka kuondoka pale nimeipiga teke sahani ya mbingu ambayo imeenda mbele na siwezi kuifikia.
Na pale nilipofungwa ni pachafu ila siwezi kupatoka.

2. (a)
- Haya ni maneno ya Kazija
- Anamwambia Maksuudi
- Wamo nyumbani kwa Kazija
- Maksuudi amekuja kumtembelea Kazija na kumfumania Mussa ambaye pia amekuja kumfuata Kazija
- Maksuudi amempiga Mussa. Mussa ametoroka
- Maksuudi amemwambia kazija kuwa yeye kazija si mwanamke,

ndipo Kazija anamwambia maksuudi maneno haya.

Hoja: 4 x 1=4

(b) (i) MAIMUNA

- Maksuudi amemzia kuufahamu ulimwengu halisi
- Alimnyima uhuru wa kuamua
- Alimtawisha kwa muda mrefu
- Alimlea kikatili
- Anamnyima elimu – anamsomeshea ndani
- Kelele zake zilimzuia kufurahia mazingira shwari
- Anamtesa kisaikolojia kwa kumtesa mamake – Tamima

(ii) TAMIMA

- Anamsaaliti kimapenzi kwa kushirikiana kimapenzi na Kazija/kusini, na Kazija
- Anamnyima uhuru wa kufurahia maisha ya ndoa – anamtusi akimwita paka.
- Alimnyima haki za binadamu kama huduma za daktari au mkunga anamkataza mkunga kuingia nyumbani mwake
- Anamwonyesha dhuluma, ukatili na hamaki – km alimpiga na kumjeruhi vibaya punde baada ya kujifungua.
- Alimtaliki bila sababu na bila kuzingatia utaratibu
- Alimfukuza usiku
- Alimzuia kufanya kazi ya ajira
- Alimnyang'anya kitoto kichanga
- Anamtawisha/anamfungia nyumbani
- Anamwacha akiwa karibu kujingua na kukaa kwa Kazija kwa Juma moja.

(iii) KAZIJA

- Maksuudi na viongozi wengine wanawanyima Kazija na wanawake wengine nafasi katika elimu.
- Anamtumia kama chombo cha starehe
- Anamdhulumu shoga yake Farashuu
- Anamdhalilisha kwa kumuuliza 'wewe ni nani'?

(iv) BITI KOCHO

- Alimdunisha
- Alimdharau
- Alimtumikisha vibaya
- Alimtisha
- Alimtusi
- Alimlipa mshahara mdogo
- Alimwachisha kazi ati kwa kosa la kumtetea Tamima
- Alimfukuza usiku.

(v) MWANASURURU

- Anamnyang'anya mali aliyoachiwa na babake
- Anamfanyia unafiki. Anamwoa kwa kutaka mali yake na kumfanya kuingilia ukahaba
- Alimtaliki baada ya kumhaini
- Alimpiga

**Mifano 4 na maelezo yake x 4=16**

3. A. Uzungumzinafsi hutokea ambapo mhusika anazungumza mwenyewe kwa mwenyewe au kimoyo moyo.

(i) Kazija anaposubiri kuja kwa Mussa na Maksuudi nyumbani kwake.
Anajisemea:"Huogopi mwanamke we! "Toka lini hata leo iwe ya pili." Labda si Kazija." Uzungumzi huu unadhihirisha azma ya Kazija na ujasiri/ukaili wa kutekeleza mpango wa Farashuu kuwafanya mtu na mwanawe kufumainiana nyumbani kwake. Jambo hili linasababisha kutengana kwa Maksuudi na mwanawe Mussa na matukio mengine yote katika riwaya.

(ii) Maksuudi anapojisemea kwa kinywa kipana "mabadiliko….!
Mwandishi ametumia mbinu hii kutubainisha hali ambapo Maksuudi anajutia matendo yake na yuko tayari kubadilika.

(iii) Maksuudi anapojiuliza "Lusu! Nani Lusu? Lusu Tamima au Maksuudi?" mwenyewe?"
Anajiuliza maswali haya akiwa shambani mdhaifu wa afya baada ya kutoka hospitali. Maksuudi anakiri makosa yake na kujutia matendo yake yaliyosababisha matatizo yaliyomkabili.

(iv) Maksuudi anaposema:"La, La, la, la… nitakwenda kuwatafuta wanangu katika uhai wangu uliobaki." Uzungumzaji huu unaashiria mabadiliko katika maisha ya Maksuudi na kusisitiza azma ya kuwatafuta wanawe. Jambo hili linaendeleza kadhia kufikia kilele/linaonyesha uwajibikaji wa Maksuudi.

**Maelezo ya uzungumzi nafsi (alama 2)**

**Hoja zozote 4 x 2=8**

B. TASWIRA
Taswira ni **picha inayojitokeza akilini mwa mtu anaposoma maandishi, anaposikiliza au kutazama jambo/mtu fulani.**

(i) Maelezo kumhusu Kazija yanayobainisha urembo wake wa kuvutia ambao unawavuta Mussa na Maksuudi na hatimaye kuwaponza na kuwatenganisha.

(ii) Maelezo kuhusu jumba la Maksuudi la kifahari lililopambwa kwa mapambo kutoka ulaya yalipopatikana kutokana na shughuli za magendo. Maelezo haya yanadokezea maovu ya Maksuudi na matendo yake hasa ya kuwatawisha mkewe na mtoto na kuwadhulumu wafanya kazi.

(iii) Taswira aliyokuwa nayo Biti Sururu ya maumbile ya Maimuna.
Maelezo haya yanaonyesha kuwa urembo wa Maimuna ulikuwa umeanza kuchujuka na hivyo kutishia chanzo cha kipato chake. Wakati ulikuwa umefika wa yeye kutafakari hatua nyingine.

(iv) Maelezo kuhusu Mussa pale alipokuwa mvunguni nyumbani kwa Kazija na vile alivyohisi akisikiliza mazungumzo kati ya Kazija na Maksuudi.

(v) Taswira ya pale hotelini
Rumbalola, yale maelezo hasa wakati Bw. Maksuudi anatokea akijikokota kumsongea Maimuna kwa furaha ya uwezekano wa kumpata mwanawe lakini Maimuna awakimbia kuzidisha utengano wao.

(vi) Taswira ya kipigo cha Tamima kutoka kwa maksuudi – kuonyesha ukatili wa Maksuudi.

(vii) Umbo/picha la tambo la Biti Kocho – kuonyesha ujasiri wake.

(viii) Maelezo kuhusu **madongoporomoka** nyumba ya Farashuu na vibanda vinavyoizunguka kuonyesha utabaka.

- Mtahiniwa ajadili mambo yanayoashiria/yanayopelekea kuanguka kwa utawala/juhudi za wanyonge kujikomboa/nyenzo zinozotumiwa na watawala kujidumisha mamlakani.

4. - Raia kususia mkutano wa Mtemi.
- Utawala kuanza kuwashuku raia na kuwasingizia mambo k.v. Mwelusi kusingiziwa kuchochea watu.
- Washauri kutowajibika huku wakisema uongo kwa Mtemi Bokono
- Manunguniko ya raia kuongezeka – k.m.dhidi ya kunyakuliwa kwa bonde la Ilangi.
- Vitisho vya watawala kwa wale wanaofikiriwa kuwa wanawachochea wananchi.

- Wasiwasi wa Bokono unaompelekea kupata majinamizi
- Viongozi kuharibu mazingira
- Matusi, ukatili, mateso na dhuluma ya watawala kwa raia k.m. Mwelusi jerezani
- Tendo la kuwaweka wananchi kizuizini – k.m. Mwelusi
- Propaganda
- Kuwajaza raia woga
- Bokono kupuuza ushauri wa Nyalwe
- Kuwalazimisha raia kutangaza uzalendo wao. Km Mwelusi kuambiwa aseme "Wapenda uongozi wa mtukufu Mtemi Bokono".
- Tenga tawala
- Kutokuwepo uelewano baina ya askari na hali kadhalika viongozi
- Utawala kuwatenganisha raia na jamaa. – Tanya kutoruhusiwa kumwona Mwelusi
- Andua, Atega – kuteka maji
- Kuimarishwa kwa shughuli za upelelezi.
- Watu kukaidi amri kama vile kuteka maji kisimani – Mwelusi, Andua, Atega kuteka maji
- Askari kupuuza amri ya kushambulia waandamanaji
- Tanya kutomwambia Batu aliko Mwelusi
- Raia kutolipwa kwa huduma watoazo – Mbutwe
- Mauaji ya Mwelusi yanapelekea kuwapo maandamano yanayomng'oa Bokono uongozini.

zozote 10 x 2=20
Kutaja -1
Mfano -1

5. (a)
- Nyalwe anazungumza na mumewe Mtemi Bokono.
- Wamo nyumbani/makao ya utawala.
- Anamdadisi kutambua ni ninikinachomsumbua.
- Anamweleza maneno aliyoyasema akiwa usingizini.

**au**

- Haya ni maneno ya Bokono – akiwa usingizini.
- Nyalwe anayakariri maneno haya kwa Bokono
- Wamo nyumbani/makao ya utawala
- Nyalwe amemwonya Bokono kuhusu uongozi mbaya
- Anamwambia Bokono ana wasiwasi wa kuondolewa mamlakani, ndipo anaota akizikwa akiwa hai.

(b) (i) Litifati: Mbinu ya kuyanukuu maneno yaliyotamkwa au yaliyosemwa na mtu mwingine. Nyalwe anayanukuu maneno ya Mtemi Bokono.

(ii) Sitiari: Ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja. Shida na matatizo/hofu ya Mtemi Bokono kulinganishwa na kaburi.

(iii) Kinaya: Mbinu ya kusema kinyume au hali kuwa kinyume na ukweli/ Mtemi Bokono ndiye anayetesa si anayeteswa/Bakono anataka kuondolewa na hali yeye anatesa.

(c)
- Mtahiniwa aonyeshe kinyume na matarajio/mambo yanayofanywa kinyume na hali inayotarajiwa.
- Utawala wa Mtemi Bokono unawatesa raia na nchi yake – kuwanyima rasilimali - maji.
- Viongozi wanatumia nafasi zao kujiendeleza – ardhi ya watoto ya kuchezea inapewa Askari Mkuu.
- Askari polisi wanawatesa raia – Mwelusi anapigwa na Talui/Mweke
- Wafungwa kunyimwa haki ya kutembelewa – Mwelusi – haruhusiwi kuonekana na Tanya.
- Raia wanalazimishwa kuhudhuria mikutano ya Mtemi Bokono.
- Raia hawana uhuru wa kumkosoa Mtemi Bokono.
- Viongozi kuharibu mazingira.
- Viongozi wanawapiganisha raia/wanachoma nyumba zao ili wapigane – Balusi/Batui
- Mtemi Bokono anajiona/anajielezea kiongozi aliyeteuliwa na Mungu
- Washauri kutomkosoa Bokono
- Utawala kuwalinda wahalifu – Askari II na kikosi hawaulizwi chochote baada ya kumuua mtuhumiwa.
- Raia kutolipwa kwa huduma.
- Askari III na II kula chakula cha mfungwa.
- Matumizi ya propaganda – Batu/Zigu kutaka kumuua Mwelusi na kutangaza kuwa amekufa kwa ugonjwa wa moyo.
- Gege kumuua Mwelusi
- Viongozi kuwatelekeza baadhi ya raia katika njaa na umaskini
- Askari III kujaribu kumnyanyasa Andua kimapenzi – anataka kumshika kifua.
- Bokono kuwa anarudi nyuma badala ya kupevuka katika uongozi.
- Nyalwe anaigiza Bokono akirudi kutoka makamo – ujana – utoto kijusi tumboni mwa mama.

6. (a) Kauli hii inatolewa na Mzee Atanasi alipokuwa njiani kutoka ofisini kwa mwalimu mkuu. Huku akiwaza, alikuwa amefika ofisini kuitikia mwito wa mwalimu mkuu. Katika mazungumzo mwalimu mkuu alimfahamisha Atanasi kubadilika kwa tabia ya mwanawe Nandwa. Mwalimu alimwomba ajaribu kumchunguza mwanawe na kusema naye ili kufahamu tatizo lake maana walimu walikuwa wameshindwa. Jambo hili lilimfanya Atanasi kuwaza mengi. (alama 4)

(b) Anayerejelewa ni Nanda mwanawe mzee Atanasi.
- Tatizo lake lilikuwa kubadilika kwa tabia kutokana na uvutaji bangi.

(alama 2)

Vitendo vya Nanda
- Kufika shuleni amechelewa
- Ulegevu
- Kusinzia darasani
- Kukosa kuzingatia usafi, kutochana nywele
- Kudorora kwa matokeo kwenye mtihani
- Kuboboja darasani
- Kupata majinamizi
- Kubumburuka usingizini na kupiga mayowe

4 x 1=alama 4

(c) Mzee Atanasi aliamini kuwa mwanawe amerogwa na jirani yake Nanda. Aliazimia pia kutafuta msaada wa waganga maarufu.

(d) (i) Malezi yasiyofaa
-Mzee Atanasi babake
-Kwa kutopata muda wa kukaa na kumchunguza mwanawe
-Alimhusu Nanda kupata ajira

(ii) Tamaa – Mzee Makulu – mwenye duka
Ndiye aliyempa Nanda kazi ya kuchuuza bangi na kumshawishi kuvuta

(iii) Unafiki – alimficha Mzee Atanasi ukweli kuhusu hali ya mwanawe.

(iv ) Kukosa mapenzi ya mama.
Mama Nanda – Mchuuzi wa samaki
Hakupata nafasi au muda wa kukaa na kumshauri mwanawe.

(v ) Hali ya umaskini ambayo ilimpelekea mtoto Nanda kuwa mhitaji hadi akatafuta ajira.

3 x 2=6

7. Mtahiniwa anahitajika kuonyesha kufanana kwa vipera hivi na vile vile kutofautiana kwake.

**Majibu**

**Kufanana**

(i) Vyote ni vipera vya semi katika fasihi simulizi

(ii) Zote ni kauli fupifupi ambazo hutoa ujumbe kwa kutumia taswira au picha
Km kitendawili nyumba yangu haina mlongo
Hapa tunaingiwa na taswira ya nyumba isiyo na mlango
Methali: Mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha mamake
Inapotajwa methali hii, tunaona picha ya mtoto aliyebebwa akitazama kisogo cha mamake

(iii) Vyote huweza kutumia lugha ya mafumbo km kitendawili
Methali: Uvivu ni nyumba ya ajizi.

(iv) Vyote huchota kutoka mazingira au jamii husika. Hutumika kutekeleza majukumu yanayofanana. Mathalan vyote hutumika kuelimisha wanajamii, kuburudisha na pia kuendeleza utamaduni wa jamii. zozote 5 x 2=10

**Tofauti**

(i) Aghalabu methali huwa na muundo wenye vipande viwili. Kipande cha kwanza huwa ni kauli ambayo hukamilishwa na kipande cha pili. Km Fahali wawili wapiganapo, nyasi ndizi huumia.

(ii) Methali huwa ni kauli nzito ambazo mara nyingi hazibadilikibadiliki.

(iii) Methali huweza kutumia tamathali nyingi za lugha kuliko vitendawili;
Km. Waweza kutumia tashihisi km Chui naye ana mke pia
Takriri: Haba na haba, hujaza kibaba.

(iv) Kimaudhui, methali huwa na maana ya juu juu na maana ya ndani
Vitendawili huwa na maana hiyo moja.

(v) Vitendawili huwa na fomula maalum ya uwasilishaji. Pana anayetega na anayetakiwa kutegua.

(vi) Vitendawili hubadilika badilika kutegemea mazingira au mpito wa wakati.

(vii) Dhima ya vitendawili si pana sana kama ya methali.

(viii) Methali huhusisha mtu mmoja lakini vitendawili huhusisha wawili au zaidi.

zozote 5 x 2=10